



**NY State of Health  
ni bima rasmi ya afya ya  
New York Marketplace.  
Je, nitajisajili vipi?**



Mtandaoni katika  
[nystateofhealth.ny.gov](http://nystateofhealth.ny.gov)



Kwa simu kupitia  
1-855-355-5777  
TTY  
1-800-662-1220



Tembelea In-Person  
Assistor kwenye  
[info.nystateofhealth.ny.gov/  
findassistor](mailto:info.nystateofhealth.ny.gov/findassistor)

NY State of Health inazingatia sheria za haki za  
raia za Shirikisho zinazotumika na haibagui kwa  
msingi wa mbari, rangi, asili ya taifa, dini, jinsia,  
umri, hali ya ndoa/familia, rekodi za kukamatwa,  
hukumu za uhalifu, utambulisho wa jinsia,  
mwelekeo wa kingono, sifa za kinasaba, hali  
ya jeshi, hali ya mhanga wa unyanyasaji wa  
nyumbani, na/au kulipiza kisasi.



Bima zote za NY State of Health zinatoa  
manufaa ya kinga ya bila malipo wa  
chunguzi na kaguzi za kila mwaka...  
**Lakini ulijua kuwa baadhi ya bima  
zinafidia ziara kwa daktari ukiwa mgonjwa  
hata ikiwa hujatimiza makato yako?**

## 1 Ziara ya ugonjwa ni gani?

- Ziara ya ugonjwa ni ziara kwa daktari wako ukiwa mgonjwa, kama vile mafua au maambukizi ya uwazi katika mfupa.<sup>1</sup>

## 2 Bima zinazofidia ziara za wagonjwa kabla ya makato hufanya kazi vipi?

- Makato ni kiwango cha pesa ambacho lazima ulipe kabla ya bima yako kufidia huduma yoyote ya afya ambayo si manufaa ya kukinga.
- Bima nyingine zitalipia ziara za ugonjwa kabla hujatimiza makato yako.**
- Hii inamaanisha unaweza kununua bima ya gharama ya chini na wewe na kila mwanafamilia wako anayefidiwa mna ziara tatu za bila malipo au za gharama ya chini za ugonjwa kwa daktari kabla ya kutimiza makato yako.
- Huenda bado ukawajibikia kutoa malipo msingi, ikiwa yapo.



### 3 Ni bima gani za NY State of Health zinafidia ziara za ugonjwa kabla hujatimiza makato?

- Mwaka wa 2020, **bima zote wastani za Shaba Nyeusi** (isipokuwa machaguo ya Akaunti ya Akiba ya Afya (Health Savings Account, HSA) zitajumuisha ziara tatu za ugonjwa za bila malipo yoyote msingi au makato.
- Baadhi ya **bima za Dhahabu na Fedha** pia zitajumuisha ziara tatu za ugonjwa kabla ya makato.<sup>2</sup>
- **Bima za Platinamu Wastani** hazina makato.

### 4 Nitapataje bima ya NY State of Health inayofidia ziara tatu za ugonjwa kabla ya makato?

Bima za afya zinazotoa huduma za ziara tatu za ugonjwa bila malipo au gharama ya chini zinapatikana katika kila kaunti.

Ili kupata maelezo zaidi:

- Tembelea zana ya ununuzi na ulinganishaji ya bima ya NY State of Health kwenye [nystateofhealth.ny.gov](http://nystateofhealth.ny.gov)
  - Tafuta bima zenye "ST3PCP" katika jina la bima.
- Tembelea msaidizi wa usajili aliyeidhinishwa bila malipo wa NY State of Health. Ili kumpata katika jamii yako:
  - Tembelea [info.nystateofhealth.ny.gov/findassistor](mailto:info.nystateofhealth.ny.gov/findassistor)
- Tupigie simu 1-855-355-5777, TTY: 1.800.662.1220.

1. Ziara za ugonjwa kwa watoa huduma msingi wanaoshughulikia matibabu ya familia, matibabu ya ndani, matibabu ya watoto, uzazi, jinakolojia, au afya ya akili kwa wasiolazwa au afya ya tabia au huduma za matumizi ya dawa za kulevya.

2. Baadhi ya huduma kama vile vipimo vya maabara, zinaweza kutolewa wakati wa ziara ya ugonjwa na zinaweza kuwa na ushiriki wa gharama au kuwa chini ya makato yako.